



**KUONGEZWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA YA MAPATO YA MWAKA YA WAFANYAKAZI KATIKA MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidial kwa Wafanyakazi (WCF) anawataarifu waajiri wote Tanzania Bara kuwa muda wa kuwasilisha taarifa ya mapato ya wafanyakazi wao (Return of Annual Earnings) kwa kipindi cha mwaka mmoja, yaani kuanzia tarehe **1 Machi 2019** hadi tarehe **29 Februari 2020** umeongezwa mpaka tarehe **30 Aprili 2020**.

Uwasilishwaji wa taarifa hizo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 73 (1) na (2) cha Sheria ya Fidial kwa Wafanyakazi [Sura ya 263 Marejeo ya Mwaka 2015] kinachotaka kila mwajiri kuwasilisha taarifa hizo kila mwaka kabla ya tarehe 31 Machi.

Kwa tangazo hili, tunawataarifu waajiri wote ambao bado hawajawasilisha taarifa hizo kuziwasilisha kwa kutumia Fomu ya Taarifa ya Mapato ya Mwaka (**WCR-3**) kwa njia ya mtandao wa kielektroniki (**Employers' Online Self-Service Portal**) unaopatikana katika kiunga cha tovuti <https://portal.wcf.go.tz>.

Aidha, Fomu ya Taarifa ya Mapato ya Mwaka (**WCR-3**) inapatikana kwenye tovuti ya Mfuko [www.wcf.go.tz](http://www.wcf.go.tz), Makao Makuu au kwenye ofisi za Mfuko za mikoani na ofisi za Kazi zilizopo mikoani na wilayani Tanzania Bara. Kwa waajiri ambao hawajaanza kutumia huduma za mtandao, Fomu zilizojazwa kikamilifu ziwasilishwe kwenye ofisi za Mfuko zilizopo ghorofa ya 6, Jengo la GEPF House, Kitalu na 37, Regent Estate-Barabara ya Bagamoyo au ofisi za Mfuko zilizopo katika mikoala mingine au ofisi za Idara ya Kazi zilizopo mikoani na wilayani Tanzania Bara.

**Imetolewa na:**

Kitengo cha Uhusiano  
**Mfuko wa Fidial kwa Wafanyakazi (WCF)**  
S.L.P 79655, Dar es Salaam

[www.wcf.go.tz](http://www.wcf.go.tz), [info@wcf.tz](mailto:info@wcf.tz)

Simu Bila Malipo: 0800110028/29